**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika;** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia uzima na afya njema, na tukaweza kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika;** Msingi wa hotuba hii ni kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 109 (15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ambayo inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza katika Mkutano wa mwezi wa Febuari au wakati mwengine ambapo Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza itaamua.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Bajeti hutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza. Aidha, Kamati huzingatia Katiba, Sheria na miongozo mbali mbali ya nchi katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara mbali mbali, Taasisi, Mamlaka, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na wadau mbalimbali kwa ajili ya kupokea taarifa za utendaji kazi na kupokea maoni mbali mbali. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Kamati imetoa maoni na ushauri kwa Serikali na taasisi hizo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi pamoja na utekelezaji bora wa

bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Bajeti imeundwa na Wajumbe sita (6) na Makatibu Kamati wanne (4) kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 8. | Ndg. Abass Vuai Mohammed | Katibu |
| 9. | Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika;** Taarifa ya Kamati ya Bajeti imegawika katika Sehemu Kuu Saba (7). **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi; **Sehemu ya Pili** ni Tathmini ya Mwenendo wa Ukuaji wa Hali ya Uchumi Zanzibar; **Sehemu ya Tatu** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 na Nusu Mwaka wa fedha 2022/2023 (Julai – Disemba 2022/2023); **Sehemu ya Nne** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Taasisi na Mashirika ya Umma; **Sehemu ya Tano** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; **Sehemu ya Sita** ni Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na **Sehemu ya Saba** ni Hitimisho.

## TATHMINI YA MWENENDO WA UKUAJI WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022

**Mheshimiwa Spika;** Mfumko wa Bei Zanzibar umeongezeka katika mwaka 2022

na kufikia wastani wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2021. Kuongezeka kwa mfumko wa bei kumesababishwa kwa kiasi kikubwa na kupanda kwa bei za bidhaa za chakula hususan mchele, unga wa ngano na sembe, ambapo mfumko wa bei wa bidhaa hizo za chakula umefikia wastani wa asilimia 12.6 kwa mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika;** Zipo sababu nyingi ambazo zimesababisha Mfumko wa Bei Zanzibar kwa mwaka 2022 kama vile kupanda kwa bei za mafuta na gesi asilia katika soko la dunia, kuathiriwa kwa kiasi kikubwa sekta ya usafirishaji ya dunia na vita vya Ukrein na Urusi, na kupanda kwa gharama za usafirishaji wa mizigo inayoletwa kutoka nje ya nchi kutokana na uwezo mdogo wa bandari ya Malindi Zanzibar kuhudumia meli za mizigo. Hata hivyo, Serikali inapaswa kuendelea kuchukua hatua madhubuti ambazo zitasaidia kupunguza kasi ya mfumko wa bei hususan kwa bidhaa za chakula.

**Mheshimiwa Spika;** Hatua hizo ni kama vile kutafuta ufumbuzi wa haraka wa changamoto ya meli za mizigo kuchelewa kufunga gati katika Bandari ya Malindi Zanzibar. Kuendeleza Miradi ya Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhia Chakula sambamba na kuanza kununua bidhaa za chakula na kuzihifadhi katika maghala hayo ili ziweze kusambazwa kwa njia ya kuuzwa kwa bei nafuu pale ambapo bei zitapanda. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa ruzuku katika nishati ya mafuta kwani inasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumko wa bei wa bidhaa hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali ianze kujenga matangi ya kuhifadhia mafuta ili kuweka akiba ya mafuta. Hatua hii itaisaidia Serikali kuwa na fursa kubwa ya kudhibiti mfumko wa bei pale bei za mafuta zitakapopanda katika soko la dunia au pale tunapokuwa na nakisi ya nishati hiyo.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Mwenendo wa Sarafu ya Tanzania, Thamani

ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine Duniani imeendelea kuwa tulivu kutokana na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti.

**Mheshimiwa Spika;** Kuhusu idadi ya watalii walioingia Zanzibar mwaka 2022, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watalii imeendelea kukua na kufikia 544,233 mwaka 2022 kutoka watalii 394,185 waliongia katika mwaka 2021. Kamati inapongeza hatua mbali mbali zinazochukuliwa ili kuongeza idadi ya watalii wanaongia nchini mwetu. Hata hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kuweka mikakati ya kuimarisha Sekta ya Utalii ili iweze kunufaika ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Utalii ina umuhimu mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi na mwananchi mmoja mmoja. Hivyo, Seikali inapaswa kuhakikisha wananchi wengi wanaendelea kushiriki kwenye shughuli za utalii kwa kuweka mikakati ya kuifungamanisha sekta hiyo na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja. Mathalan, Serikali inaweza kuviwezeshwa vikundi vya wajasiriamali kuzalisha bidhaa zinazotumika katika hoteli za kitalii kama vile mboga mboga, viungo vya chakula nakadhaalika. Hatua hii itasaidia kuongeza ajira sambamba na kuimarisha uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022 NA NUSU MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI – DISEMBA 2022/2023)

**Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha uliyopita yaani 2021/2022, Serikali ilifanikiwa kukusanya asilimia 79 ya makadirio ya mapato iliyopanga kukusanya. Kwa upande wa Mwenendo wa Mapato na Matumizi kwa Nusu Mwaka wa 2022/2023 (Julai – Disemba 2022/2023), Kamati imeelezwa kwamba Serikali imefanikiwa kukusanya asilimia 91 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika;** Licha ya kwamba Serikali imekuwa ikiendelea kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Kamati inaona Serikali inayo fursa kubwa ya kuongeza mapato yake maradufu iwapo itachukuwa hatua zifuatazo: Kuendelea na hatua za kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato

na mifumo ya manunuzi kwa njia za kielektroniki ili kuendelea kudhibiti uvujaji wa mapato na kudhibiti manunuzi ya holela.

**Mheshimiwa Spika;** Hatua nyengine ambazo zitasaidia kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa pamoja na kuweka mikakati Madhubuti ya kuhakikisha mashirika ya umma na kampuni za Serikali yanajiendesha kwa faida ili hatimae yaweze kutoa gawio kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Kuhusu Tathmini ya Deni la Taifa, hadi kufikia Disemba 2022, Deni la Taifa linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) limefikia TZS 331.9 bilioni na lile linalodhaminiwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar limefikia TZS 2,368.1 bilioni. Hii inafanya jumla ya Deni la Taifa kufikia TZS 2,700 bilioni.

**Mheshimiwa Spika;** Deni hili bado ni himilivu lakini kasi yake ya kuongezeka ni kubwa sana. Serikali inapaswa kuchukua hatua za kupunguza kasi ya ukuaji wa deni kama vile kuongeza ukusanyaji wa mapato, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuendelea kutafuta misaada na inapokuwa hakuna budi kukopa basi tukope mikopo isiyokuwa ya kibiashara. Aidha, Serikali inapaswa kutokuendelea kukopa fedha ZSSF kwa sababu majukumu ya ZSSF ni kukusanya fedha za wanachama wake na kuziwekeza ili iweze kutengeneza faida.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA

**Mheshimiwa Spika;** Ili kubaini kiasi cha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Mashirika ya Umma, Mamlaka na Kampuni za Serikali, Kamati ya Bajeti ilizitembelea baadhi ya taasisi hizo na kubaini mambo yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Mamlaka ya Mapato Zanziabr (ZRA), Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ZRA kushindwa kuunganisha mifumo ya

hoteli za kitalii katika mifumo ya kodi. Katika hili, Kamati inaishauri, ZRA kufanya tafiti za namna taasisi za kukusanya kodi katika nchi za jirani na za visiwa kama Zanzibar zinavyotekeleza majukumu yao ya kukusanya kodi katika hoteli za kitalii na maeneo mengine ya kitalii ili kuongeza mbinu na ujuzi wa namna kuongeza mapato kutoka katika sekta ya utalii.

**Mheshimiwa Spika;** Kuhusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Mkoa wa Kikodi Pemba inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa nafasi katika Bandari za Mkoani na Wete pamoja na uhaba wa nyenzo za kushushia mizigo kutoka katika meli, hali ambayo inapelekea wafanyabiashara kutokuingiza mizigo moja kwa moja kutoka nje ya nchi. Aidha, changamoto nyengine ni kuwepo ugumu wa kupata taarifa halisi za mapato wanayolipwa wafanyakazi wataalamu kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika;** Ili kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri mambo yafuatayo: Kwanza, ili kuleta ufumbuzi wa haraka kwa ufinyu wa nafasi katika bandari za Pemba na uhaba wa nyenzo za kushushia mizigo kutoka katika meli, Kamati inaishauri Serikali kufanya mazungumzo ya kushirikiana na Mamlaka ya Mapato ya Kenya (KRA) ili wafanyabiasha wa Pemba waweze kuitumia Bandari ya Mombasa. Aidha, ili kuleta ufumbuzi wa kudumu, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza kwa haraka Miradi ya Kuimarisha Bandari za Mkoani na Wete.

**Mheshimiwa Spika;** Jambo la pili ambalo Kamati inashauri ili kutatua changamoto ya kuwepo ugumu wa kupata taarifa halisi za mapato wanayolipwa wafanyakazi wataalamu kutoka nje ya nchi ni kuanzishwa kwa vitengo vya Ukaguzi wa Kiuchunguzi (Forensic Audit) sambamba na kuvijengea uwezo kwa kuwapa mafunzo ya kutosha watendaji wake. Hatua hii inapaswa kutekelezwa na ZRA na TRA ili kutatua changamoto kuwepo ugumu wa kupata taarifa halisi za mapato wanayolipwa wafanyakazi wataalamu kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika;** Taasisi nyengine ambayo Kamati ya Bajeti imeona itowe msisitizo kwa kuitaja kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi yetu ni

Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC). Shirika hili linakabiliwa na changamoto kubwa na za muda mrefu ambazo zinaathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya uchumi wetu. Baadhi ya changamoto ambazo Kamati imebaini zinalikabili Shirika la Bandari ni kama zifuatazo: Meli za mizigo kutoka nje kukaa nangani kwa muda mrefu zikisubiri kushusha makontena katika Bandari ya Malindi. Meli hizi zimekuwa zikisubiri kwa takriban siku 33 na hivyo kusababisha gharama za usafirishaji mizigo (freight) kupanda. Na changamoto nyengine ni ukosefu wa eneo la kutosha la kuhifadhia makontena hali inayopelekea msongamano wa mizigo katika Bandari ya Malindi.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kutatua changamoto za Shirika la Bandari, Kamati inaishauri Serikali itekeleze kwa haraka mpango wa kuanzisha bandari kavu (ICD) sambamba na kuendelea na mipango ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Bandari Mpya ya Mangapwani. Aidha, Serikali ikiwa inaendelea na mikakati ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu kuhusu changamoto ya meli za mizigo kusubiri muda mrefu, Kamati inaishauri Serikali ifanye utafiti wa namna ya kuchimba (dredging) katika bandari ya Mkoani Pemba ili iweze kuhimili meli zenye kina (draft) cha mita 11.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa Mashirika ya Umma, Mamlaka na Kampuni za Serikali nyengine ambazo Kamati ilipata fursa ya kufanya nayo kazi ilibaini kuwepo kwa changamoto zinazofanana. Changamoto kubwa ambazo Kamati imebaini ni kuwepo kwa ufahamu mdogo wa matumizi ya Mfumo wa Manunuzi kwa njia ya kielektroniki hali inayochangia kukwama kwa taratibu za manunuzi. Changamoto nyengine ni uhaba wa fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu yao na uhaba wa watendaji, kukosa majengo kwa ajili ya ofisi pamoja uhaba wa vyombo vya usafiri.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kuweka msisitizo wa maelezo haya, naomba niyataje baadhi ya Mashirika, Mamlaka, Kampuni hizo zinazokabiliwa na

changamoto hizo kama ifuatavyo: Mamlaka Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA), Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC), Kamati ilipokutana na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA), Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI), Kampuni ya Mwani Zanzibar (ZASCO), Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS), Shirika la Meli Zanzibar, Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC), Shirika la Magazeti, na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA),

**Mheshimiwa Spika;** Ili kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali iendelee na mafunzo ya matumizi ya mfumo wa manunuzi wa kielektroniki kwa watendaji wote wanaohusika na kazi za manunuzi katika taasisi za Serikali ili mfumo huo uweze kufahamika na kuweza kutumika ipasavyo. Aidha, Kamati inawashauri watendaji wote kuacha visingizio kwa lengo la kuvunja moyo matumizi ya mfumo wa manunuzi, jambo la muhimu ni kuondoshwa kwa changamoto zilizopo lakini kutumia mfumo hakuna mbadala wake.

**Mheshimiwa Spika;** Katika changamoto ya uhaba wa fedha za ruzuku na fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Mashirika, Mamlaka, Kampuni za Serikali. Kamati imebaini kutokuwepo kwa uwiano wa ongezeko la mapato na upatikanaji wa ruzuku na fedha za matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilitegemea kwa vile mara kwa mara kunaripotiwa kuongezeka kwa mapato na muda mwengine kuvukwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato, kungelikuwa na ongezeko la kiasi cha ruzuku na matumizi mengineyo (OC) kwa taasisi za Serikali. Kamati inaisisitiza Serikali kuliangalia suala hili la uhaba wa fedha za ruzuku na fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa umakini mkubwa kwani linakwamisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo. Ili taasisi hizi ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuongeza makusanyo ya mapato, Serikali inapaswa kuwekeza katika taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika;** Kuhusu changamoto ya uhaba wa watendaji, kukosa majengo kwa ajili ya ofisi pamoja uhaba wa vyombo vya usafiri, Kamati inashauri kufanyike tathmini ya kina kwa Mashirika, Mamlaka, Kampuni za Serikali kuhusiana na mahitaji ya rasilimali watu. Afisi ya Rais – Katiba inapaswa kutoa vibali vya ajira pale inapojiridhisha kuwepo kwa uhitaji wa kuajiri watendaji wapya kwa ajili Mashirika, Mamlaka, Kampuni za Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Tunahitaji Mashirika, Mamlaka, Kampuni za Serikali zijiendeshe kwa ufanisi ili ziweze kupata faida na kutoa gawio kwa Serikali. Hivyo, Mashirika, Mamlaka, Kampuni za Serikali hizi zinahitaji kuwa na watendaji wa kutosha wenye uwezo na weledi wa kutekeleza majukumu ya taasisi hizo kwa ufanisi.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA PROGRAMU MBALI MBALI

**Mheshimiwa Spika;** Katika kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023, Kamati ya Bajeti ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji katika baadhi ya Miradi ya Maendeleo na Programu mbali mbali iliyomo katika Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 sambamba na kufanya ziara katika maeneo ya miradi hiyo ili kutathmini kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo, thamani ya fedha zinazotumika pamoja na kubaini changamoto zinazoibuka wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika;** Baadhi ya Programu na Miradi hiyo ya Maendeleo ni kama hii ifuatayo: Miradi na Programu zilizotekelezwa kwa Fedha za Ahueni ya UVIKO 19 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Maabara ya Taasisi ya Viwago Zanzibar (ZBS), Mradi wa Ujenzi wa Marekebisho ya Bandari ya Mkoani Pemba, Mradi na Ujenzi wa Bandari ya Shumba, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima, Mradi wa Mpango wa Utayarishaji wa Matumizi ya Ardhi, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya KMKM, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya KVZ, Progaramu ya Umwagiliaji Maji, Programu ya Ujenzi wa

Barabara za Ndani pamoja na Matengenezo ya Barabara za Mjini, Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria, Programu ya Uimairishaji wa Viwanja vya Ndege na Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu kwa Barabara ya Chake Chake - Wete na Chake Chake – Mkoani,

**Mheshimiwa Spika;** Katika utekelezaji wa Miradi na Programu zilizotekelezwa kwa Fedha za Ahueni ya UVIKO 19 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), kumejitokeza kasoro mbali mbali kama vile baadhi ya miradi kupangiwa fedha zaidi ya mara moja. Mathalan, Mradi wa Kuwawezesha Vijana Wanaoacha Dawa za Kulevya umepangiwa fedha katika fungu la fedha za Sekta ya Uwezeshaji na fungu la fedha za Shughuli za Uratibu. Jambo hili linaathiri hesabu ya jumla kuu. Kamati inaishauri Serikali kutoa uchambuzi na ufafanuzi wa fedha zilizotumika katika miradi na shughuli zote zilizotekelezwa kwa fedha za UVIKO 19. Aidha, katika ufafanuzi huo kuwepo na maelezo ya fedha zilizoripotiwa zaidi ya mara moja kwa shughuli au mradi moja.

**Mheshimiwa Spika;** Kasoro nyengine iliyojitokeza katika utekelezaji wa Miradi ya Fedha za Ahueni ya UVIKO 19 ni kutumika kwa fedha nyingi kwa ajili ya kazi za kawaida za kiofisi kama vile kuwajengea uwezo watendaji na ununuzi wa stationaries, saver, printers, photocopy machines na computers, honda “click”, jenereta na gari. Fedha za mikopo kama hizi za UVIKO 19 zilipaswa kutekeleza kazi za maendeleo tu na sio shughuli za kawaida ambazo inawezekana kugharamiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaisisitiza Serikali kutumia fedha za mikopo kwa ajili ya kazi za maendeleo tu. Haileti taswira nzuri kwa fedha za mikopo kutumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za kawaida kama vile kuwajengea uwezo watendaji au kununua stationaries, kompyuta nakadhaalika. Jambo hili ni kinyume hata na agizo la Serikali wenyewe la kutaka taasisi zisitumie fedha za UVIKO 19 kwa kazi au shughuli zisizo za maendeleo, hata mikataba ya Washauri Elekezi iliagizwa isainiwe na Afisi ya Rais – Fedha na Mipango ili malipo yake yasitokane na fedha za UVIKO 19.

**Mheshimiwa Spika;** Changamoto nyengine ni kutokupelekwa kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu na badala yake zimewekwa Benki ya CRDB na kuelekezwa ZAFICO kuzikopa na kuzitumia kununua boti za uvuvi. Jambo hili ni kinyume na taratibu za kibajeti. Matumizi yote yanapaswa kuidhinishwa na Katibu Mkuu kama ilivyoelekezwa na Baraza la Wawakilishi wakati wa kupitisha vifungu vya bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika;** Tathmini ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo inaonesha kuwa Programu na Miradi mingi inakabiliwa na changamoto za kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi, kuchelewa kwa malipo ya fidia za majengo na miti na wakandarasi kuwa na uhaba wa vifaa vya ujenzi. Serikali inapaswa kufanya tathmini ya namna utekelezaji wa Programu na Miradi inavyotekelezwa. Kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi kunapelekea kuchelewa kumalizika kwa miradi jambo ambalo huleta hasara kubwa kwa Serikali kwa sababu vifaa vya ujenzi vinapanda bei kila baada ya muda lakini pia miradi ikichelewa huathiri ustawi wa nchi yetu. Hali hii ndio huifanya miradi kuwa mzigo kwa Serikali badala ya kuwa kitega uchumi au kichecheo cha ukuaji wa uchumi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati imebaini sababu kubwa ya kuwepo kwa changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi katika Programu na Miradi ya Maendeleo ni kuwepo kwa utitiri mkubwa wa miradi, jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi mingi hutekelezwa kwa asilimia ndogo au kutokutekelezwa kabisa kutokana na kukosa fedha. Tunapanga miradi mingi lakini tunatekeleza kwa kiwango kidogo sana.

**Mheshimiwa Spika;** Ili kutatua changamoto ya wakandarasi kuwa na uhaba wa vifaa vya ujenzi, Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha inasimamia agizo lililotolewa kwa wakandarasi kuhusiana na uletaji wa vifaa vya kutosha ili kuepusha uzoroteshaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya

fidia za majengo na miti kwa wananchi walioathiriwa na utekelezaji wa miradi, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuwalipa fidia kwa haraka iwezekanavyo kabla ya kuanza kwa mradi husika.

**Mheshimiwa Spika;** Progaramu ya Umwagiliaji Maji ni miongoni mwa programu ambazo Kamati imeweka msisitizo kutokana na kutokuridhishwa na utekelezaji wake licha ya kwamba fedha nyingi zimeshatumika kugharamia programu hii. Katika Programu ya Umwagiliaji, eneo la kazi lilipunguzwa hasa kwa mabonde ya Pemba lakini katika upande wa fedha kulikuwa na nyongeza.

**Mheshimiwa Spika;** Progaramu ya Umwagiliaji Maji inatekelezwa kwa Mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 50 (sawa na TZS 115 bilioni) kutoka Benki ya Exim Korea. Fedha hizi ni nusu ya Fedha za Ahueni ya UVIKO 19 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambazo zimetekeleza miradi mingi sana inayoonekana na kuleta tija kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inawakumbusha watendaji kwamba kinachopima mafanikio katika miradi kama hii ni uzalishaji (yields) na sio maelezo ya nadharia kama vile mabonde mangapi yamemaliza kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji na visima vingapi vimechimbwa.

**Mheshimiwa Spika;** Programu nyengine ambayo Kamati imeona itoe msisitizo kutokana na umuhimu wake ni Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani pamoja na Matengenezo ya Barabara za Mjini. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na mkakati mpya wa kugharamia miradi ya barabara kwa kutumia mfumo wa EPC + Finance. Katika mfumo huu, barabara zinatengenezwa kwa mikopo baadae Serikali italipa taratibu badala ya kutumia utaratibu wa awali wa kujenga kwa fedha za ndani hali inayopelekea miradi ya ujenzi wa barabara kutekelezwa kwa kasi ndogo mno. Pamoja na kuanzisha mfumo huu katika utekelezaji wa miradi ya barabara, Kamati inaishauri, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuongeza umakini katika kusimamia miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa vile Mkataba wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani unaeleza kutumika kwa utaratibu wa mfumo wa EPC + Finance katika utekelezaji wake. Kwa utaratibu huu mkandarasi alitakiwa kutumia fedha zake kulipia gharama za ujenzi lakini katika mkataba huu kuna kipengele cha kulipwa gharama za awali (advance payment) ya USD 8 milioni. Kamati inaishauri Serikali inapoingia mikataba ya EPC + Finance ihakikishe inafata taratibu za mikataba hiyo na kuepuka kulipa fedha za awali.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kubaini ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na bajeti za Serikali za Mitaa hususan katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Maeneo Maalum kwa Wajasiriamali, Mradi wa Ujenzi wa Stendi za Magari na Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Daladala. Kamati ilizitembelea Halmashauri, Mabaraza ya Miji na Manispaa zote kwa Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika;** Katika utekelezaji wa miradi hiyo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikabiliwa na changamoto zifuatazo: Fedha za ahueni ya UVIKO 19 ambazo ndizo zilizogharamia miradi hiyo hazikuhusisha gharama za kumlipa Mshauri Elekezi, na kutokuwepo kwa Upembuzi Yakinifu uliofanyika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaishauri Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, gharama za malipo ya Mshauri Elekezi zitengwe kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwezesha kupatikana kwa Mshauri Elekezi kwa utaratibu uliopangwa. Aidha, Kamati inaisisitiza Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kutokuchelewesha marejesho ya mapato yanayoingia Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo yanakusanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kuchelewesha kurudisha mapato ya Mamlaka hizo ni kuzifanya zishindwe kutekeleza

majukumu yake kwa ufanisi.

## TATHMINI YA HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YATOKANAYO NA TOZO ZA MAEGESHO YALIYOPO KATIKA WILAYA YA MJINI HUSUSAN MAENEO YA MASOKO NA MAENEO MAALUM YA MAEGESHO

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilielezwa kwamba, Manispaa ya Mjini imeingia mkataba wa ubinafsishaji wa huduma ya maegesho na Kampuni ya ECONEX katika maeneo yote ya Manispaa ya Mjini. Mgao wa Manispaa ya Mjini ni asilimia 60 na kampuni ya ECONEX ni asilimia 40 ya makusanyo. Kamati inapata wasiwasi mkubwa juu ya mgawanyo wa mapato. Kwa msingi huo, Kwanza Manispaa ya Mjini haina uhakika wa kiasi kitakachokusanywa. Pili, ubinafsishaji hufanyika pale ambapo taasisi imeshindwa kutoa huduma husika. Je, Manispaa ya Mjini inashindwa kuweka usimamizi na kukusanya mapato ya maegesho katika maeneo yake?

**Mheshimiwa Spika;** Kwa lengo la kuongeza mapato na kuongeza ajira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati inaishauri Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Unguja na Pemba kuanza taratibu za kukusanya wenyewe mapato katika maeneo ya maegesho ya gari na masoko. Jambo hili linahitaji kuwa na watendaji wenye weledi wa ukusanyaji mapato sambamba na kutumia mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki ili kuzuia uvujaji wa mapato hayo.

## Maoni ya Ujumla

**Mheshimiwa Spika;** Miongoni mwa masuala ambayo Kamati yangu inahitaji kuyatolea maoni ya jumla ni Mashirika ya Umma na Kampuni za Serikali kutowasilisha taarifa zake za mapato na matumizi ya kila mwaka katika Baraza la Wawakilishi. Jambo hili ni matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika;** Kuwepo kwa changamoto ya kutokufahamu kutumia Mfumo

wa Manunuzi kwa njia ya Kielektroniki kumeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya taasisi nyingi za Serikali pamoja utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfumo wa Manunuzi ni njia nzuri ya kudhibiti matumizi ya Serikali lakini kumekuwa na malalamiko mengi ya kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa namna ya kutumia mfumo huo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka Ununuzi (ZPDDA) kufanya mafunzo kwa taasisi zote zenye uhitaji wa mafunzo sambamba na kuanzisha dawati maalum la kutoa msaada iwapo taasisi hizo zitapata changamoto wakati wa utumiaji wa mfumo.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande mwengine Kamati inazitaka taasisi zote kutumia mfumo wa manunuzi na iwapo kutatokea changamoto yoyote waombe msaada Mamlaka ya Ununuzi. Aidha, wakati wa kupewa mafunzo ya mfumo wa manunuzi kwa maafisa manunuzi na watendaji wengine wanaohusika na manunuzi, Kamati inashauri maafisa TEHAMA nao washiriki ili waweze kusaidiana na maafisa manunuzi wakati wa kutumia mfumo huo.

**Mheshimiwa Spika;** Suala jengine ambalo Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali ni kutengeneza bajeti zenye uhalisia, mara nyingi kunapangwa kutekelezwa miradi mingi lakini baadae inashindikana kuingiziwa fedha au utekelezaji wake unakuwa wa kusuasua.

**Mheshimiwa Spika;** Suala la mwisho ambalo Kamati ya Bajeti inasisitiza ni kushindwa kwa Mashirika ya Umma na Kampuni za Serikali kujiendesha kwa faida na hatimae kuweza kutoa gawio kwa Serikali. Serikali inapoteza kiasi kikubwa cha mapato kutokana na Mashirika na Kampuni za Serikali kutokutoa gawio kabisa au kutoa kiasi kidogo. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya uendeshaji wa Mashirika na Kampuni zote umma ili iweze kuja na mikakati madhubuti ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo.

## HITIMISHO

Naomba nihitimishe kwa kukushukuru Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid kwa

kuliendesha Baraza hili la Wawakilishi kwa weledi mkubwa. Pia namshukuru Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika kwa kukusaidia vyema katika kutekeleza majukumu yako.

Aidha, napenda kuwashukuru Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizofanya kazi na Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yao mazuri na hatimae kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao muda wote wakati wa kutekeleza shughuli za Kamati.

Kamati inaishukuru kwa dhati kabisa Afisi ya Baraza la Wawakilishi na watendaji wake wote ambao waliweza kuisaidia Kamati katika kufanikisha kazi zake na kupatikana kwa ripoti yake kwa wakati uliopangwa.

Kwa kumalizia, Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa Wizara na taasisi zote za Serikali kutekeleza maagizo na ushauri wa Kamati zote waliopatiwa ili kuimarisha utendaji wa Wizara na taasisi hizo na kupatikana kwa matokeo mazuri ya usimamizi wa Kamati kwa taasisi hizo.

Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa lipokee na kujadili ripoti hii ili hatimae Serikali iende kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Baraza kwa ujumla.

Naomba kutoa hoja.

………………………………….
Mhe. Abdulla Hussein Kombo,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**